Nipashe Uk. 5, Tarehe 05/06/2021

# Serikali yapiga marufuku usafirishaji wa nguruwe

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

NGURUWE 12 wamethibitika kufa kutokana na homa ya nguruwe Manispaa ya Morogoro na serikali imepiga marufuku usafirishaji wa wanyama hao na nyama yake kutoka nje ya mkoa huo.

Aidha, kata tano kati ya 29 za Manispaa ya Morogoro zimethibitika kuathiriwa na ugonjwa huo.

Ofisa Mifugo wa Manispaa ya Morogoro, Dk. Petro Lema, alithibitisha hilo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuwa ugonjwa huo hauna madhara kwa binadamu atakekula nyama ya nguruwe aliyeathiriwa.

Alisema walipata taarifa ya kuibuka kwa ugonjwa huo Juni 2 na kuchukua sampuli kuzipeleka maabara ya chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na kubaini kuwapo kwa vimelea vya ugonjwa huo kwa nguruwe waliokufa katika kata za Kingolwira, Tungi, Kichangani, Boma na Kilakala.

Dk. Lema alisema uchunguzi wa awali wamebaini kuwa ugonjwa huo kutokea mkoani Dodoma na Manispaa ya Morogoro ulianzia kata ya Kingolwira na idara ya mifugo kwa kushirikiana na jeshi la polisi tayari wameshaweka vizuizi katika mpaka wa barabara ya Iringa, Dodoma na Dar es salaam ili kuzuia wafanyabiashara kuingiza au kutoa wanyama hao.

Alisema wanaokula nyama hiyo kwenye vibanda, mabucha na baa hawaruhusiwi kubeba mabaki kupelekea mifugo nyumbani ili kuepuka ugonjwa huo kusambaa.

"Tumeendelea kutoa elimu kwa makundi mbalimbali wakiwamo wauzaji wa kitoweo cha nguruwe, wafugaji na wauzaji chakula cha mifugo, ugonjwa huu unasababishwa na kirusi na hautibiki," alisema.

Pia, alisema atakayekiuka masharti atachukuliwa hatua ikiwamo kutozwa faini ya Sh. 200,000 na watakaobainika kuwa na nyama hiyo bila mihuri, nyama itateketezwa.

## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya GADAU AUCTION MART AND COMPANY LTD, MASE INTERNATIONAL LTD na MAK RECOVERIESLTD Kwa idhini tuliyopewa na FINCA MICROFINANCE BANK LTD tunatoa muda wa siku 14 kwa wadaiwa walioorodheshwa kwenye jedwali hapo chini wawe wamelipa madeni wanayodaiwa na FINCA MICROFINANCE BANK LTD, kinyume na hapo tutalazimika kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara mali walizoweka kama dhamana ya mkopo. Tarehe za kufanya minada zitatolewa kwa njia ya vipeperushi na magari ya matangazo kwenye sehemu dhamana zilipo.

| S/N | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA |
|---|---|---|---|
| 1 | Charles Nyuka Mhoja | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Mazengo Magya - Morogoro Mjini |
| 2 | Alex Mwasigwa Bulenga | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Kihonda - Barabara ya Mazimbu - Morogoro |
| 3 | Juma M. Mussa | Gari aina ya Nissan Caravan Na ya usajili T785 DLC | Morogoro Mjini |
| | | MAK RECOVERIES LTD | |
| | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA |
| 4 | Godfrey Saledi Mhu | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Chumbageni - Tanga Mjini |
| 5 | Salimu Abdallah Bori | Lori aina ya Ual Tractor Multicolor yenye namba za usajili T 386 CLS na Trailer Multicolor yenye namba za usajili T 157 BKS | Duga Maromboni Tanga Mjini |
| 6 | Halima Omar Hoza | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | |
| 7 | Elizabeth Mshomvu | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Amboni Mafuriko,Tanga Mjini |
| 8 | Ruth O Sakala | Samani za nyumbani | Mpwapwa -Dodoma |
| 9 | Emmanuel V Ngonda | Nyumba yenye mkataba wa mauziano na Mitsubishi canter yenye namba ya usajili T350 ABB | Kwa mama John - Mbeya |
| 10 | Fides A Mhogela | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Mwakapangala Mbalizi - Mbeya |
| 11 | Mansour Alfuman Mbarouk | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Mwanjelwa - Mbeya |
| 12 | Jackson A Mwalyego | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Iyunga - Mbeya |
| 13 | Cecilia J Sinkala | Samani za biashara na samani za nyumbani | Ituha - Mbeya Mjini |
| 14 | Neema Hassan Ambonisye | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Mbeya |
| 15 | Burton W Chombe | Nyumba iliyopo kiwanja namba 218, Kitalu D, Mbalizi mbeya | Mwanyimbe - Isanzi<br>Mbalizi - Mbeya |
| | | MASE INTERNATIONAL LTD | |
| | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA |
| 16 | Diana Stevene Kilara | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Kebibari - Tarime |
| 17 | Thomas Mhonya Mayalla | Nyumba yenye hati, kiwanja namba 148, Kitalu E Mayengo kahama mjini | Mayengo - Kahama Mjini |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Dhamana itauzwa kama ilivyo, mahali ilipo.
3. Mnunuzi atayeshinda anapaswa kulipa 25% ya bei aliyofikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia atalipa ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada, kinyume na hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha Hati miliki (Transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa ni la mnunuzi.
5. Mnada utafanyika mahali ambapo dhamana zilipo na si vinginevyo.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA NAMBA**

Mkurugenzi Mtendaji
Gadau Auction Mart and Company Limited
P.o.box 40855
Dar es Salaam

Na
Mkurugenzi Mtendaji,
Mack Recoveries Ltd
0715 375475/ 0783224965
0716 35 3650/0783 481 798

Na
Mkurugenzi mtendaji,
Mase international Ltd
P.O. Box 6797
Mwanza

Na
Finca Microfinance Bank Ltd
P.O. Box 78783
Namba 0768790399, 0754774549

Scanned with CamScanner

# Watanzania washauriwa kuongeza ulaji wa nyama

NA MWANDISHI WETU

PAMOJA na kuwa na mifugo mingi, Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo Wananchi wake hawali nyama kwa wingi kama inavyoshauriwa kiafya.

Msajili wa Bodi ya Nyama nchini Dk. Daniel Mushi alisema kuwa takwimu zinaonesha kuwa katika kipindi cha mwaka 2020/2021Tanzania ilizalisha zaidi ya tani laki saba za nyama ikiwa ni wastani wa kilo 15 kwa kila Mtanzania kwa mwaka.

Dk. Mushi aliongeza kuwa Shirika la Afya Duniani (WHO), limekuwa likishauri kila mtu kula kilo 50 za nyama kwa mwaka, kiasi anbacho kwa Tanzania haijafikia hata kwa nusu.

Aidha, Dk. Mushi alibainisha kuwa nyama nyekundu ni muhimu kwa afya ya binadamu, ingawa si nzuri sana kula zaidi ya gramu 70 kwa siku, kutokana na kuwa na madini mengi ya chuma.

Akizungumzia changamoto mbalimbali zinazoikabili Bodi ya Nyama Nchini, Dk. Mushi alitaja miongoni mwa changamoto hizo kuwa ni kutokuwa na takwimu sahihi za ulaji wa nyama kwa kuwa bado watu wengi wamekuwa wakichinja mifugo majumbani mwao.

Scanned with CamScanner

# Mawaziri SMZ, Muungano wakubaliana maeneo 8 mifugo

**Na Gloria Tesha**

WIZARA zinazohusika na mifugo katika Serikali ya Muungano na Zanzibar zimepitisha maazimio manane ya ushirikiano katika kuimarisha sekta hiyo ikiwamo kutambua vibali vya pande zote mbili vya kusafirisha mifugo, kuchochea uwekezaji na kuboresha ufugaji.


Katika maazimio hayo, wataalamu wa wizara hizo wamekubaliana kufanya maboresho katika sheria, miongozo na kanuni za mifugo kuongeza kasi ya kuifanya sekta kutoa ajira nyingi na kufungua fursa zaidi za uingizaji wa vifaranga wazazi kutoka nje ya nchi kwenda Zanzibar.

Akizungumza jana baada ya kukamilika kwa kikao cha wataalamu wa wizara hizo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Mifugo), Profesa Elisante Ole Gabriel, alisema hatua hiyo ni utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan wa Tanzania na Dk Hussein Mwinyi wa Zanzibar kuhusu ushirikiano wa sekta zisizo za Muungano.

"Tumekubaliana kurahisisha kutambua vibali vya kusafirisha mifugo kama kimetolewa Zanzibar kitambulike Bara na cha Bara kitambulike Zanzibar, wasitoe hongo wala rushwa Takukuru wapo kazini. Kuna namna tunaweza kuokoa zaidi ya shilingi bilioni 161.4 kama tukiunganisha nguvu kudhibiti magonjwa kwani asilimia 60 ya magonjwa ya binadamu yanatoka kwa wanyama," alisema Profesa Ole Gabriel.

Maazimio ya ushirikiano ni katika kuanzisha na kuendeleza malisho ya mifugo; katika utafiti wa magonjwa ya mifugo, mbegu bora za mifugo na malisho ya mifugo; kudhibiti uingizaji wa bidhaa, mazao ya mifugo nchini hususan maziwa na nyama ya kuku; kudhibiti magonjwa yasiyo na mipaka; na kutoa mafunzo ya mifugo.

Mengine ni ushirikiano katika kutoa elimu kwa wafanyabiashara, wasafirishaji na wadau wanaohusika kusafirisha bidhaa kati ya Serikali ya Muungano na Zanzibar na kuwajengea uelewa wa sheria na kanuni za kisekta watumishi wanaofanya kazi katika sekta; uzalishaji wa mifugo hususan kuifanya Zanzibar kituo cha kuzalisha mitamba ya ng'ombe chotara; na udhibiti wa taaluma na huduma za Veterinari.



Katibu Mkuu, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Zanzibar, Maryam Juma Saadalla alisema maazimio hayo yatatekelezwa sambamba na kuhakikisha Zanzibar inapata vifaranga wazazi kutoka nchi ziziso na athari za mafua ya ndege na kuwataka wafugaji wa Tanzania Bara kwenda Zanzibar kuwekeza kwani fursa ni kubwa.

Habari Leo Uk. 3, Tarehe 05/06/2021

Scanned with CamScanner

# Uvuvi haramu wadhibitiwa asilimia 80

Na Matern Kayera

SERIKALI kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imedhibiti uvuvi haramu kwa asilimia 80 kwenye maji baridi yakiwemo maziwa, mito na mabwawa.

Pia imedhibiti uvuvi haramu kwa asilimia 100 kwenye maji chumvi hususan Bahari ya Hindi ambako aina kubwa ya uvuvi haramu iliyokuwa ikitumika ni ya kutumia milipuko ya baruti.

Hayo yamebainishwa na Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulika na Uvuvi, Dk Rashid Tamatamaha alipozungumza na HabariLeo kuhusu Siku ya Kimataifa ya Kudhibiti Uvuvi Haramu ambayo huadhimishwa kila mwaka Juni 5 (leo).

Alisema uvuvi haramu ni dhana pana ambayo pamoja na kuhusisha matumizi ya nyavu zisizoruhusiwa, pia inahusisha kitendo cha mtu kuvua bila kuwa na leseni, kutumia chombo cha uvuvi ambacho hakijasajiliwa na utoroshaji wa samaki kwenda nje ya nchi.

Dk Tamatamah alisema pamoja na serikali kufanikiwa kwa kiasi kikubwa kudhibiti uvuvi haramu, changamoto ya matumizi ya makokoro, watu kuvua bila leseni na utoroshaji wa samaki kwenda nje ya nchi bado zipo japo kwa kiasi kidogo.

"Kabla ya mwaka 2017 hali ilikuwa mbaya sana, lakini mwaka 2018 Idara kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama, waliendesha operesheni mwaka mzima ikiwemo Operesheni Sangara Ziwa Victoria na Operesheni Jodari Bahari ya Hindi ambazo zilifanikiwa kuondoa nyavu haramu, na kwenye bahari tulikamata meli moja ya uvuvi Mtwara ya kutoka Vietnam na wahusika walifungwa," alisema Dk Tamatamah.

Operesheni hiyo ilifanyika kwenye maziwa yote na maeneo ambayo yalikuwa na maji ya kawaida na kufanikiwa kudhibiti uvuvi haramu kwa asilimia 80 kwenye maji baridi yakiwemo maziwa, mito na mabwawa na asilimia 100 kwenye bahari.

Wakati akiwasilisha bungeni hivi karibuni Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa Wizara yake kwa mwaka 2021/2022, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alisema wavuvi wadogo huchangia asilimia 95 ya samaki wote wanaovuliwa nchini na asilimia tano iliyobaki huchangiwa na wavuvi wakubwa.

Habari Leo, Tarehe 05/06/2021

Scanned with CamScanner

# RC ahimiza ufugaji wenye tija

Na Veronica Mheta,Monduli

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongela amewataka maofisa mifugo na watendaji wa halmashauri kuhimiza ufugaji bora na wa kisasa huku wakihakikisha majosho yanaongezwa na kushawishi ujenzi wa viwanda vya bidhaa za mifugo kuinua uchumi .

Mongela alielezea haja ya watendaji wa vijiji na kata kuwezeshwa zaidi katika mambo mbalimbali kwani wao ni viungo muhimu vya upatikanaji wa taarifa zitazoiwezesha serikali kupanga mikakati ya maendeleo ya maeneo husika.

Mongela alisema hayo jana wilayani Monduli wakati akizungumza na baadhi ya viongozi wa halmashauri hiyo katika ziara yake ya ukaguzi wa miradi mbalimbali itakayozinduliwa na Mwenge wa Uhuru kwenye wilaya hiyo.

Alisema siyo lazima wafugaji wakalazimishwa kulima ilhali wamezoea kufuga hivyo ni vema waboreshewe mazingira ya ufugaji sambamba na ujenzi wa viwanda .

Alihimiza kuboresha majosho na masoko ya minada ya wafugaji ili waone manufaa ya kufuga na ndipo elimu ya kilimo itolewe ili wapate chakula

Mkurugenzi wa halmashauri ya Wilaya ya,Monduli Stephen Ulaya alisema ushauri wa Mkuu wa Mkoa utazingatiwa kwani wilaya hiyo ilikuwa inategemea utalii katika kukusanya mapato lakini sasa utalii umeshuka kwa sababu ya ugonjwa wa covid 19.

Habari Leo Uk. 19, Tarehe 05/06/2021

Scanned with CamScanner

# Watanzania washauriwa kuongeza ulaji wa nyama

NA MWANDISHI WETU


PAMOJA na kuwa na mifugo mingi, Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo Wananchi wake hawali nyama kwa wingi kama inavyoshauriwa kiafya.

Msajili wa Bodi ya Nyama nchini Dk. Daniel Mushi alisema kuwa takwimu zinaonesha kuwa katika kipindi cha mwaka 2020/2021Tanzania ilizalisha zaidi ya tani laki saba za nyama ikiwa ni wastani wa kilo 15 kwa kila Mtanzania kwa mwaka.

Dk. Mushi aliongeza kuwa Shirika la Afya Duniani (WHO), limekuwa likishauri kila mtu kula kilo 50 za nyama kwa mwaka, kiasi anbacho kwa Tanzania haijafikia hata kwa nusu.

Aidha, Dk. Mushi alibainisha kuwa nyama nyekundu ni muhimu kwa afya ya binadamu, ingawa si nzuri sana kula zaidi ya gramu 70 kwa siku, kutokana na kuwa na madini mengi ya chuma.

Akizungumzia changamoto mbalimbali zinazoikabili Bodi ya Nyama Nchini, Dk. Mushi alitaja miongoni mwa changamoto hizo kuwa ni kutokuwa na takwimu sahihi za ulaji wa nyama kwa kuwa bado watu wengi wamekuwa wakichinja mifugo majumbani mwao.



Mkurugenzi wa Utafiti, Mafunzo na Ugani kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Angelo Mwilawa akieleza kuhusu malisho ya nyasi zilizoandikwa na "Hey" kama yanavyojulikana kitaalam wakati timu ya wafugaji na wazalishaji wa malisho ya mifugo kutoka mikoa ya Njombe, Mbeya, Tanga na Kilimanjaro walipofika kwenye shamba la kikundi cha Mkaff kilichopo kijiji cha Ngarenairobi Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro jana.

# Serikali yawataka wafugaji kujiunga kwenye vyama vya ushirika

NA OMARY MTAMIKE

SERIKALI imewataka wafugaji kote nchini kujiunga na vyama vya ushirika ili waweze kutekeleza shughuli zao za ugani kwa tija.

Hayo yamesemwa leo (03.06.2021) mkoani Kilimanjaro na Mkurugenzi wa Utafiti, Mafunzo na Ugani Dkt. Angelo Mwilawa wakati akihitimisha ziara ya siku 7 ya wafugaji na wazalishaji wa vyakula vya mifugo kutoka mikoa ya Njombe, Mbeya, Tanga na Kilimanjaro.

Dk. Mwilawa amebainisha kuwa kupitia ushirika wafugaji na wazalishaji wa malisho ya mifugo wataweza kupata huduma zao zote za msingi kwa urahisi ikiwa ni pamoja na pembejeo na zana mbalimbali ambazo wanaweza kuzitumia kwenye shughuli zao za ugani.

"Kwa mfano tumeona wilaya ya Hai kuna ushirika ambao umefanikiwa kununua mashine na kuweka kiwanda cha chakula bora cha mifugo jambo ambalo limewasaidia wafugaji waliopo kwenye ushirika huo kupata chakula cha mifugo yao na tumeona hata uzalishaji wa maziwa kwa wafugaji hao umeongezeka kwa asilimia 20 zaidi tofauti na ilivyokuwa hapo awali" Ameongeza Dk. Mwilawa.

Dk. Mwilawa ametoa rai kwa watanzania wenye nia ya kufanya biashara kuchangamkia fursa ya biashara ya malisho ya mifugo kwa sababu mahitaji yake ni makubwa ikilinganishwa na kiwango kinachohitajika.

Kwa upande wake mmoja wa washiriki wa ziara hiyo kutoka mkoani Njombe, Rahel Mhema ameishukuru Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kuwawezesha kushuhudia kile kinachofanywa na wafugaji wenzao katika mikoa mingine ambapo ameomba kuongezeka kwa ziara za aina hiyo ili waendelee kuongeza ujuzi zaidi katika kazi hiyo ya ufugaji.

"Nitoe wito na rai kwa vijana na wanawake wenzangu kuanza kufanya shughuli hii ya ufugaji kwa sababu una faida kubwa na unamfanya mfugaji kupiga hatua za maendeleo kadri siku zinavyoenda" Amesema Mhema.

Naye Kiongozi wa Shirika la kimataifa la utafiti wa malisho (CIAT), An Notenbaert amesema kuwa amefurahi kuona namna wafugaji na wazalishaji wa malisho walivyoweza kuboresha mifugo yao na kuongeza kiwango cha uzalishaji wa maziwa kupitia malisho yaliyoboreshwa ambapo amewasisitiza kuendelea kutunza mazingira wakati wote wa utekelezaji wa shughuli zao.

Mbali na wafugaji na wazalishaji wa malisho, ziara hiyo pia ilihusisha wataalam kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi na viongozi mbalimbali wa vyama vya ushirika vya wafugaji kutoka katika maeneo waliyotokea washiriki hao.

Scanned with CamScanner